# MIKAKATI YA KUBORESHA SHUGHULI ZA LISHE HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA 2019/2020

| NA. | IDARA | MKAKATI WA KUBORESHA LISHE |
|---|---|---|
| 1 | **AFYA** | ❖ Kutenga fedha kwenye bajeti ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe (Shilingi 1000/ kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano<br>❖ Utoaji wa Elimu ya lishe katika ngazi mbalimbali hasa kwa akina mama wenye watoto wenye umri wa miezi 0 hadi 23<br>❖ Kuibua na kutibu utapiamlo mkali kwa watoto wa umri wa chini ya miaka 5 ( Idara imetenga jumla ya shilingi 9,696,869.70 kwa ajili ya kununulia chakula dawa<br>❖ Kuendeleza maonyesho ya mapishi ya vyakula vya watoto wenye umri wa kuanzia miezi 6 – 59 katika siku za afya za vijiji na kupitia redio Sibuka<br>❖ Kujadili masuala ya lishe kwenye vikao vya kamati mseto ya lishe wilaya<br>❖ Kuwashirikisha watendaji wa kata na vijiji katika masuala ya lishe kwa kila robo<br>❖ Kusambaza vipeperushi na machapisho ya lishe katika kata zote 36 na vituo vya kutolea huduma za afya<br>❖ Kufuatilia juu ya utekelezaji wa mikataba ya lishe kwa watendaji wa Kata na Vijiji ikiwemo na utoaji wa taarifa juu ya viashiria vya lishe |

| NA | IDARA | MKAKATI WA KUBORESHA LISHE |
| --- | --- | --- |
| | **AFYA** | ❖ Kumshirikisha Mkuu wa Wilaya katika masuala ya lishe ili katika mikutano yake ngazi ya jamii aweze kusisitiza juu ya elimu ya lishe<br>❖ Kuishirikisha CMT katika suala la lishe ili isaidie kueneza elimu ya lishe<br>❖ Kushirikiana na wadau wa lishe katika kutekeleza afua za lishe.<br>❖ Utoaji wa vitamini A pamoja na dawa za minyoo kwa watoto wenye umri wa miezi 6 -59 |
| | | |
| 2 | **KILIMO NA USHIRIKA** | ❖ Kuendelea na uhamasishaji wakulima kutumia mbolea na mbegu zilizoidhnishwa na Taasisi pamoja na kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya kanuni bora za kiliom ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na kuzifanya kaya ziwe na uhakika wa chakula<br><br>❖ Uhamasishaji kwa wakulima kulima mazao yanayostahimili ukame na jinsi ya kuhifadhi bora ya chakula ikiwa na uhamasishaji wa kilimo cha bustani kwenye maeneo yenye uhakika wa maji |

| NA | IDARA | MKAKATI WA KUBORESHA LISHE |
|---|---|---|
| 3 | **MIFUGO NA UVUVI** | ❖ Kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa kwa kupandisha ng'ombe 500 kwa njia ya chupa katika kata za Shanwa, Nyalikungu, Malampaka, Sola, Ng'wigwa, Zanzui, Kadoto, Binza Seng'waBusilili, Mbaragane na Buchambi.<br><br>❖ Kuendelea kutoa elimu ya kanuni bora za ufugaji ikiwemo chanjo ya ugonjwa wa chambavu na kimeta kwa ng'ombe pamoja na chanjo ya ndui na kideri kwa kuku katika mikutano ya vijiji, lengo ikiwa ni kuongeza upatikanaji wa kiini lishe cha utomwili.<br><br>❖ Kuendeleza ufugaji wa samaki kwenye malambo ya watu binafsi na ya serikali lengo likiwa ni kuongeza kiinilishe aina ya utomwili na madini.<br>❖ Kuendelea kutoa huduma ya kukagua mifugo inayochinjwa katika machinjio zote za Wilaya ya Maswa, lengo ikiwa ni kuhakikisha jamii inapata nyama iliyo bora hivyo kuongeza kiwango cha utomwili na kuepusha jamii kupata magonjwa yatokanayo na ulaji wa nyama.<br><br>❖ Kuendelea kufanya mikutano ya uhamasishaji vijijini juu ya matumizi ya makundi matano ya vyakula,ikiwepo matumizi ya chumvi yenye madini joto na matumizi ya virutubishi vya madini chuma na vitamin ya foliki Asidi kwa akinamama wajawazito na wanaonyonyesha |

| NA | IDARA | MIKAKATI YA KUBORESHA LISHE |
| --- | --- | --- |
| 4 | **ELIMU MSINGI** | ❖ Kuendelea Kutoa elimuya lishe kwa walimu wa afya mashuleni ili elimu hii iwafikie wanafunzi ambao nao wataifikisha kwenye jamii<br>❖ Kuhakikisha shule zote 121 zinalima viazi lishe ekari 3 kwa kila shule kwa ajili ya kuboresha afya za wanafunzi na jamii kwa ujumla na kupata mali ghafi kwa ajili ya kiwanda cha viazi lishe<br>❖ Kuhamasisha wazazi kupitia kamati za shule kulima viazi lishe ili watoto waweze kula viazi wakiwa nyumbani pamoja na kupata mali ghafi kwa ajili ya kiwanda cha viazi lishe |
| | | |
| 5 | **ELIMU SEKONDARI** | ❖ Kuendeleza kilimo cha mazao ya chakula (Mahindi na Mtama) katika shule zote 36 za sekondari za serikali ili wanafunzi wawe wanapata chakula shuleni<br>❖ Kuhamasisha wazazi kuchangia chakula kwa ajili ya kuwezesha wanafunzi wapate chakula shuleni<br>❖ Kuishirikisha Idara ya Kilimo ili kuziwezesha kitaalamu shule za sekondari Binza na shule ya wasichana Maswa kuanzisha kilimo cha bustani |

## MIKAKATI YA KUBORESHA HALI YA LISHE

| NA | IDARA | MIKAKATI YA KUBORESHA LISHE |
|---|---|---|
| 6 | **MAENDELEO YA JAMII** | ❖ Kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu masuala ya lishe na usafi wa maji na mazingira kupitia mikutano ya hadhara na WDC<br>❖ Kuhamasisha na kutoa elimu juu ya lishe kupitia makundi ya WAVU,vijana, akina mama na watu wenye ulemavu<br>❖ Kuendelea kutoa elimu ya lishe kwa watendaji wa Kata / vijiji na wanufaika wa TASAF |
| | | |
| 7 | **MIPANGO** | ❖ Kusimamia utengwaji wa fedha kwenye mipango na bajeti kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya Afua za lishe. |
| | | |
| 8 | **TEHAMA** | ❖ Kuhabarisha jamii juu ya masuala yahusuyo lishe |
| | | |